

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge
S.L.P. 941
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi Moja (11) unatarajiwa kuanza kesho Jumanne tarehe 06 Septemba 2016 na kumalizika tarehe 16 Septemba 2016 Mjini Dodoma. Shughuli zitakazokuwepo katika Mkutano huo ni kama ifuatavyo:-

1.0 MASWALI

Katika Mkutano huo jumla ya maswali ya kawaida 110 yanatarajiwa kuulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali 16 ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yanatarajiwa kuulizwa pia.

2.0 MISWADA YA SHERIA:

Katika Mkutano wa Tatu wa Bunge Miswada sita (6) ya Sheria ilisomwa mara ya Kwanza na kupelekwa kwenye Kamati husika ili ifanyiwe kazi. Hivyo katika Mkutano wa Nne Miswada hiyo itashughulikiwa katika hatua zinazofuata (Kusomwa mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu). Miswada hiyo ni:-

- (i) Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa mwaka 2015 (*The Access to Information Bill, 2015*),
- (ii) Muswada wa Sheria ya Utathimini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016*).

- (iii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 (*The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016*).
- (iv) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataluma wa Kemia wa mwaka 2016 (*The Chemist Professionals Bill, 2016*).
- (v) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016*).
- (vi) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa Mwaka 2016 (*The Tanzania Fisheries Institute Bill, 2016*).

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano.

Ofisi ya Bunge

DODOMA.

05 Septemba, 2016.